# NI VYEMA KUWA NA MATAMANIO MATAKATIFU ( SHAUKU) UNAPOKWENDA MBELE ZA BWANA. MAANDIKO: WAAM. 6:11-14 NA 1SAM. 1:9-11.

1. **UTANGULIZI**

Kama kuna jambo la pekee ambalo Mungu analiangalia ndani ya moyo wa mteule ambaye anakwenda mbele zake; jambo hilo ni yale matamanio matakatifu anayokuwa nayo mteule ndani ya moyo wake (shauku). Matamanio au kiu au shauku ya kutaka kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, matamanio ya kutaka kuona jambo fulani au adui anapigwa ili Yesu apate kutukuzwa; au upate jambo fulani kwa ajili ya utakatifu wa Mungu; hili ni jambo ambalo Mungu hulifurahia sana na kutenda jambo haraka kabisa. (kusikia kilio hicho haraka sana)

**Mfano:-**

a. **Gideoni** matamanio yake (shauku) yalikuwa ni kuyaona matendo makuu ambayo amehubiriwa na Baba zake. Hataki Mungu abakie wa historia tu bali adhihirike na kuwapigania tena Waisrael na kuwaondoa katika utumwa waliokuwa wanatumikishwa na Wamidiani- Matamanio haya ndiyo Bwana Yesu aliyoyaona ndani ya moyo wa Gideoni na akashuka na kuyafanya matamanio aliyokuwa anadai ***Waam. 6:11-14, 7:9-25, 8:22-23.*** Mataminio (shauku) takatifu ya kutaka kuyaona matendo makuu ya Mungu katika maisha yake ikamfikisha kuwa mtawala/ mwamuzi wa Israeli muda wa miaka 40!! ***Waam. 8:28*** ( shauku ya Gidioni **ilikuwa ni hii yako wapi matendo makuu ya Mungu wa Israeli?? Akayaona!!**

b. **Mwanamke HANA -** Alikuwa na shauku (matamanio) ya kumpata mtoto wa kiume ili amtoe sadaka kwa Mungu ili awe Mtumishi wa Mungu siku zake zote atakazoishi hapa duniani!! ***1Samwl. 1:9-11***. Mungu akaona matamanio haya ya ajabu kwa mwanamke huyu; na Mungu akafanya na zaidi. ***1Samwl. 1:17-20, 3:1-11, 15-21, 12:1-7, 25:1***. Alivyotamani mama yake (shauku) ndivyo Samweli alivyotumika siku zote za maisha yake hadi kifo chake; Mungu akatukuzwa sana kwa kuzaliwa kwa mtoto Samweli duniani, lakini na mama (Hana) naye akaburudishwa moyo wa Mungu na kumfanya **acheke** na kuimba Zaburi. ***1Samwl. 2:1-11***

c. **Mfalme Daudi :** shauku ya Daudi ( Matamanio yake) ni kumuua Goliath ili kuwaondolea Israeli aibu ya kutukanwa na wapagani au kumjengea Mungu nyumba nzuri ili sanduku la Bwana lisikae katika mahema tena na Bwana akambariki sana kwa matamanio haya. ***1Samwl 17:22-26, 32-37, 45-48, 2Samwl 7:1-2***

d. **Yakobo mkwewe Laban.** Baada ya kufanya kazi ya kuchunga wanyama wa Baba mkwe wake kwa muda wa miaka 20 na kuishi ukweni, **Yakobo akatamani sasa moyoni mwake aangalie mambo ya nyumba yake yeye mwenyewe** ( kuangalia ni pamoja na kuwajibika kama Baba kwa familia kwa mambo ya kimwili pamoja na kiroho) ***Mwanz. 30:25-43 ( Mwanz. 31:38-42)***

- Pamoja na Yakobo kuchunga wanyama wa Baba mkwe wake miaka (20) alikuwa analipwa mshahara mdogo na muda wote alipata mateso mengi kwa kushinda porini pamoja na masimango mengi kutoka kwa Baba mkwe wake; akatamani moyoni mwake aangalie mambo ya familia yake, na Bwana akainglia kati haraka na kumfariji sana hadi Baba mkwe wake akaanza kumwangalia kwa jicho la hila na wivu tele!!. ***Mwanz 31:1-16***

- Hali hiyo ya Labani kumnyanyasa Yakobo (mkwewe) hata watoto wake (Lea na Raheli) waliiona, na hata wakaamua kuungana mkono na Yakobo (mume wao) na wakaondoka maana hawana urithi tena katika nyumba ya Baba yao (**mst 14-16**) " **And Rachel and Lea answer him and said "Is there yet any portion or inheritance for us in our father's house? Are we not counted by him as strangers? For he sold us and has also quite devoured our money (the price you paid for us). For all the riches which God has taken from our father are ours and our children's. Now then whatever God has said to you, do it.** Yakobo anamaliza safari yake kama Baba ambaye ameacha Baraka tele kwa watoto wake na hata wajukuu wake.
  ***Mwanz. 48:8-22, 49:1-33* 28-33***. **Aliacha alama ya ajabu sana duniani hadi leo- kabila 12 za Israel**

e. **Zakayo mtoza ushuru-*Luk. 19:1-10*** yeye alitamani ndani ya moyo wake kumwona Yesu huyu ni mtu wa namna gani?

- Inawezekana kabisa Zakayo alikuwa amepata ushuhuda wa kuponywa na Yesu kipofu maarufu katika mji wa Yeriko aliyekuwa omba omba maarufu na yeye Zakayo alikuwa miongoni mwa watu  waliokuwa wakimpa sadaka (***Luk. 18:35-43).*** Kwa hiyo akaweka kando heshima yake na kupanda juu ya mkuyu kwa matamanio ( shauku) ya kumwona Yesu ni mtu wa namna gani huyu hata anatenda mambo ambayo madaktari bingwa hawawezi!! Yesu aliona shauku ya moyo wa Zakayo na akaamua kwenda kushinda nyumbani mwaka  hadi watu ( Mafarisayo) wakanung'unika!! Na Yesu akawa rafiki wa Zakayo na Zakayo akawa ni miongoni mwa wanafunzi wa Yesu wa siri wa ajabu sana. Kweli Zakayo alimwona Yesu asiye na ubaguzi wala kubeza wenye dhambi na akashinda naye nyumbani mwake tendo ambalo baadhi ya wanafunzi wa Yesu hawakulipata ingawa walizunguka naye miaka $3^{1/2.}$

f. **Yabesi** -***1Nyak. 4:9-10.*** Yabesi (huzuni) ni mtoto ambaye mama yake alimzaa katika mateso na taabu nyingi; hatujui hata jina la Baba yake kwa sababu inawezekana mama yake alipachikwa tu mimba kama watoto wa mitaani walivyo leo na  kisha kumwacha mama huyu akihangaika na mimba hadi alipozaa na kumwita mtoto Yabesi (Huzuni)

- Yabesi akaonewa na kuchekwa na wengi kutokana na hali yake ya maisha aliyokuwa akiishi. Yabesi aliposikia habari za Mungu pamoja na ukuu wake; Biblia inasema akamlingana Mungu wa Israeli

  " **Ampl Bible- Jabez cried to the God of Israel saying- oh that you would bless me indeed and enlarge my border and that your hand might be with me and you would keep me from evil so it might not hurt me! And God granted him that which he requested**. ( Yabesi alilia mbele za Mungu wa Israeli, shauku ya moyo wake ilikuwa ni kumwona Mungu wa Israeli akimtoa katika hali ile ya unyonge na kumbariki na kuwa pamoja naye na kwamba baraka atakazopata zisimwondoe kwa Bwana na Bwana akatenda. Elewa kwamba Yabesi wala mama yake hawakuwa Waisraeli!! Ndiyo sababu anamlingana Mungu wa Israeli

  **Note: Vilio vyetu vinalenga nini tunapokuja mbele zake!!**

g. **Mariamu Magdalena:** ***Yoh. 20:1-18(10-18)*** wakati Mariamu Magdalena anakwenda kaburini na Petro na Yohana,alfajiri na mapema tofauti yake na Petro na Yohana ni shauku zao (matamanio yao). Yeye alilia na anataka kujua Yesu yuko wapi baada ya kukuta kaburi liko wazi na Yesu hayumo na yuko tayari kumchukua na kwenda naye nyumbani mwake; Petro na Yohana wao wanataka kushuhudia tu kwamba Yesu hayumo kaburini halafu waende zao na kupiga hadithi na mitume wenzie!!

- Angalia mistari hii kwa makini – ***Yoh. 20:11-18-*** "Mama unalila nini" " Malaika waliona kilio cha Mariamu cha ndani sana; lakini hata Yesu anakiona kilio cha ndani cha upendo wa ajabu na wapekee kabisa ndani ya moyo wa Mariamu Magdalena tofauti na wanafunzi wale wengine na Yesu naye akamuuliza swali lile lile aliloulizwa na malaika " mama unalilia nini" kisha akaamua kujidhihirisha kwake
- Mungu anaangalia shauku ya ndani (Matamanio) na kamwe hajidhihirishi kwa watu ilimradi tu wanaomba au wako katika kusanyiko la wapendwa!! ***Yoh. 2:23-25***

**Note: Hata kama wewe ni kipofu, tasa, maskini, mgonjwa watoto wako wameharibiwa na dunia, ndugu zako uwapendao hawajaokoka, biashara yake imeyumba sana, madeni mengi unaonewa na kunyanyaswa na kubezwa, bila ya kuwa na shauku/ matamanio kama Musa kwanza** ***(Kut. 2:11-14,*** ***( Ebr. 11:23-27)*** **alitamani kuona ndugu zake wanakuwa huru!! Batholomayo alitamani aone kwa macho yake mawili; Mwanamke msamaria akatamani kuona ndugu zake wasamaria wanatuliwa mizigo yao, na Yesu akawaokoa kwa jisi ya ajabu-** ***Yoh. 4:28-30;*** **halafu** ***Yoh. 4:39-41*****!! Shauku/ matamanio yangu yako matakatifu ni yapi mwaka 2022!! Mfano wa Nyerere na Mandela waliokuwa na shauku na nchi zao kuwa HURU!!**

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***02/1/2022***